*JARIDA LA CHALUFAKITA*
*Juz. 5, 2023, 42-63*

# UTEKELEZAJI WA MTAALA UNAOEGEMEA KATIKA UWEZO KUPITIA FASIHI : MAONI KUTOKA KWA WALIMU NA WANAFUNZI KATIKA SHULE TEULE ZA SEKONDARI

Donard Bikorimana
Chuo Kikuu cha Rwanda
bpatientdona@gmail.com

na

Willy Migodela
Chuo Kikuu Katoliki Ruaha
migodela@rucu.ac.tz

**Ikisiri**

*Makala hii inaijadili fasihi kama nyenzo mwafaka ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kutokana na stadi za karne ya 21, masuala mtambuka, na maadili na mwenendo mwema kupewa uzito katika mtaala huu. Wango la utafiti lilikuwa ni walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika kidato cha tano katika shule teule za sekondari nchini Rwanda pamoja na kazi za fasihi zinazotumiwa na walimu wakati wa ufundishaji. Sampuli ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Nadharia ya Mwingiliano wa Tamaduni-jamii iliongoza hatua mbalimbali za utafiti ulioibua haja ya kuandika makala hii. Aidha, ukusanyaji wa data ulitumia mbinu ya ushuhudiaji, uchambuzi wa matini na mahojiano. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kwamba fasihi hutoa mifano mwafaka ya uwezo wa jumla, masuala mtambuka na mitazamo na thamani. Kwa hivyo, sifa hii sio tu inaifanya fasihi kuwa nyenzo mwafaka ka ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo bali pia kudhihirisha umuhimu wa nyuga za kiinsia hata katika zama za sasa.*

## 1.0 Utangulizi

Kwa sasa, nyuga za kiinsia zinakabiliwa na changamoto ya kupoteza umuhimu wake. Tatizo hili linatokana na maendeleo pamoja na mabadiliko ya kiuchumi. Aidha, elimu inayosisitizwa ni ile inayoshughulika na ufundishaji wa mambo muhimu katika ufanikishaji wa shughuli za kiuchumi na siyo yale yenye umuhimu lakini yasiyohusiana na faida za moja kwa moja za kiuchumi. Pamoja na hayo, mifumo ya kielimu inatarajiwa kutawaliwa na michakato ya ufundishaji na

ujifunzaji ambayo itakuza uwezo unaohitajika katika zama za sasa. Uwezo huo ni ule wa kumjenga mhitimu atakayekuwa mshindani bora kwenye soko la ajira la kiulimwengu (UNICEF, 2019). Hali hii imeibua matumizi ya mtaala unaoegemea katika uwezo kwa sababu ndio unalenga kukuza uwezo unaohitajika katika ulimwengu wa kisasa.

Kwa mujibu wa Nzima (2016) mtaala unaoegemea katika uwezo unaweza kutazamwa kama aina ya mtaala unaolenga kuwezesha wanafunzi kukuza, kuunganisha na kutumia uwezo unaohitajika kama vile utatuzi wa matatizo, tafakuri tunduizi, ubunifu, teknolojia ya habari, ushirikiano na ujifunzaji usio na mpaka. Aina hii ya mtaala inasisitiza uwezo ambao wahitimu wanaweza kutumia katika shughuli tofauti za kazi na maisha katika jamii zao badala ya kulenga tu kupata maarifa. Mtaala huu unasisitiza kile ambacho wanafunzi wanatarajiwa kufanya badala ya kuzingatia zaidi kile wanachotarajiwa kujua (Kabombwe na Mulenga, 2019). Hata hivyo, tunaweza kusema kuwa katika ufundishaji na ujifunzaji unaoegemea mtaala huu, nguvu hupaswa kuwekwa katika matendo ya ujuzi na maarifa ya mwanafunzi kutokana na kile alichojifunza kuliko kushangilia ujuzi na maarifa aliyonayo.

Mtaala unaoegemea katika uwezo unashughulikia vipengele muhimu vitatu ambavyo ni pamoja na uwezo wa jumla ambao pia hurejelewa kama stadi za karne ya 21, masuala mtambuka na mitazamo na thamani (REB, 2015). Vipengele hivi vinajumuisha miktadha yote ya kimaisha ambapo utendaji wa ujuzi na maarifa hufanyika. Ijapokuwa katika muhtasari wa Kiswahili wa REB (2015), wanatumia istilahi "maadili na mwenendo mwema" badala ya mitazamo na thamani. Katika makala hii ni bora kutumia "mitazamo na thamani" kwa sababu ndiyo istilahi inayoakisi mada yetu vema zaidi.

Aidha, fasihi kwa ujumla (fasihi andishi na fasihi simulizi) huzingatia maisha halisi ya watu katika miktadha yote ya kimaisha na hivyo kuifanya jamii kutilia maanani uga wa fasihi (Duhan, 2015). Kwa mujibu wa Duhan (khj) fasihi pia inatoa mifano ya kufungua uwanja wa utendaji wa ujuzi na shughuli za kimaisha. Kutokana na mtaalamu huyu, ni dhahiri kwamba fasihi inazingatia na kushughulikia uwezo wa jumla, masuala mtambuka na mitazamo na thamani. Vipengele hivi ni muhimu katika mtaala unaoegemea katika uwezo.

Tangu mtaala unaoegemea katika uwezo uanzishwe nchini Rwanda, unakabiliwa na changamoto za ukuzaji wa uwezo wa jumla miongoni mwa wanafunzi na ujumuishaji wa masuala mtambuka katika kila somo (Nsengimana, 2021). Aidha, Lazar (1993) katika Hapsari (2011) anaeleza kuwa fasihi ni nyenzo isiyo ya kufundishia lugha tu bali hukuza uwezo wa mwanafunzi na kujumuisha mitazamo na thamani kwa watumizi wake. Hata hivyo, hakuna maandiko wala tafiti

zinazoeleza kwamba fasihi inaweza kuwa nyenzo mwafaka ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo. Hivyo basi, utafiti uliofanyika ulichunguza namna fasihi inavyoweza kufaa na kutumiwa kama nyenzo ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kupitia wanafunzi wa lugha katika shule za sekondari nchini Rwanda, wilayani Rusizi.

Hivyo basi, makala hii inajielekeza katika kushughulikia kwa kina suala la utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Makala inashughulikia suala hili kwa kubainisha uhusiano uliopo kati ya fasihi na vipengele vya mtaala unoegemea katika uwezo. Makala inatathmini ufaafu wa fasihi kama nyenzo ya kufundisha vipengele vya mtaala unaoegemea katika uwezo. Pia, makala inaeleza jinsi fasihi inavyoweza kuwa nyenzo mwafaka ya kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo. Kwa upande wa nyuga za kiinsia, makala inapendekeza kuwa walimu na wanafunzi pamoja na wadau wengine wa nyuga hizi kutekeleza vizuri mtaala unaoegemea katika uwezo kama utetezi mzuri wa umuhimu wa nyuga za kiinsia. Bila shaka, utetezi wa namna hii, utakuwa na mashiko zaidi kuliko ule wa kutegemea zaidi huruma kuhalalisha umuhimu wa nyuga za kiinsia.

## 2.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Mwingiliano wa Tamaduni-jamii iliyoasisiwa na Lev Vygotsky mnamo 1920 na 1930. Nadharia ya Vygotsky inazingatia sana ukuzaji wa tafakuri tunduizi na utumizi wake katika utatuzi wa matatizo, upangaji, utengenezaji wa maana, tukitaja kwa uchache (Fahim na Haghani, 2012). Nadharia hii inaeleza kuwa utambuzi binafsi wa mwanadamu unakuzwa kupitia ushirikiano wa kijamii na shughuli za kitamaduni. Ni dhahiri kwamba msingi huu unasisitiza ukuzaji wa uwezo binafsi wa mwanafunzi pamoja na utendaji wake katika maisha halisi. Hili ndilo lengo kuu la mtaala unaoegemea katika uwezo ambalo linatarajiwa kufikiwa kwa kila mwanafunzi. Kwa hivyo, Nadharia ya Mwingiliano wa Tamaduni-jamii na fasihi zote huzingatia nafasi ya uwezo wa kibinafsi pamoja na mchango wa mazingira katika ufanikishaji wa shughuli za maisha.

Nadharia ya Mwingiliano wa Tamaduni-jamii inazingatia Mwingiliano tofauti yanayoweza kujitokeza kati ya mwanafunzi na nyenzo za ujifunzaji kwa njia ya upatanishi na muktadha wa kijamii. Kwa maneno mengine, nadharia hii inashughulikia suala la zana ambazo mtu anatumia kujifunza, wapi ujifunzaji hufanyika, na kwa nini mtu huyo anajifunza. Misingi ya mtaala unaoegemea katika uwezo nayo huzingatia malengo ya ujifunzaji, mazingira na nafasi ya nyezo za ujufunzaji katika ufikiaji wa malengo ya ujifunzaji. Fasihi nayo inashughulikia mazingira halisi ya binadamu, maendeleo yake na nyenzo zinazoweza kumsaidia katika maendeleo yake. Hivyo basi, misingi hii ilitusaidia kukusanya na kuchambua data zinazohusiana na nafasi ya fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea

katika uwezo. Wazo hili lilitokana na msisitizo unaowekwa na mtaala unaoegemea katika uwezo wa kumpa mwanadamu misingi ya kimaendeleo maishani.

Nadharia hii ilichaguliwa kutokana na sifa zake muhimu mbili: Mosi, ni sifa ya kusisitiza ujifunzaji wa mtu binafsi, mchango wake na utofauti wake katika mchakato wa ujifunzaji. Aidha, mtaala unaoegemea uwezo husisitiza pia ubinafsi wa mtu na ushirikiano wake na wengine katika kujenga jamii. Hali hii ilitusukuma kuoanisha hoja za msingi huu na zile za mtaala unaoegemea uwezo, tukaona kwamba ni mwafaka katika ufikiaji wa lengo la utafiti wetu. Hata hivyo, misingi ya nadharia hii inaweka mkazo katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi ya mtu na ubunifu wake katika ujifunzaji wa somo maalumu.

Pili, Nadharia ya Mwingiliano wa Tamaduni-jamii ina sifa ya kusisitiza utendaji wa ujuzi katika mazingira na maisha halisi ya kijamii. Sifa hii inaweka kipaumbele katika utumiaji wa ujuzi alionao mtu katika ufanikishaji wa shughuli za kimaisha, hususan zile za kiuchumi. Sifa hii inahusiana moja kwa moja na ile ya mtaala unaoegemea katika uwezo ya kumjengea mwanafunzi uwezo wa kuchangia katika uchumi wa kijamii. Kutokana na sifa hizi mbili za Nadharia ya Mwingiliano wa Tamaduni-jamii, tuliona inafaa kuongoza utafiti wetu kikamilifu.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Eneo la kijiografia katika utafiti wetu lilikuwa ni shule za sekondari zinazofundisha fasihi ya Kiswahili wilayani Rusizi nchini Rwanda. Shule za sekondari zilichaguliwa kutokana na sababu ya kwamba ndicho kiwango cha awali ambacho hushughilikia ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda. Lakini kitu cha muhimu zaidi ni kwamba shule za sekondari hushughulikia tanzu zote mbili za fasihi yaani fasihi simulizi na fasihi andishi katika Kiswahili.
Wilaya ya Rusizi nayo ilichaguliwa kutokana na eneo lake la kijiografia ambapo rai wake wengi huongea lahaja ya Kiswahili-Kingwana. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba huwa na athari tofauti za ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa wilaya hii. Eneo la kitaaluma ni baadhi ya kazi za fasihi andishi na fasihi simulizi zinazopatikana katika vitabu vya Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha tano nchini Rwanda.

Sampuli ya utafiti huu ilipatikana kwa kutumia usampulishaji usio nasibu hususani usampulishaji lengwa. Kwa mujibu wa Dornyei (2007), katika usampulishaji lengwa tunapaswa kufanya baadhi ya maamuzi yenye kanuni kuhusu jinsi ya kuchagua washiriki wetu, wakati wa kuongeza washiriki wa ziada kwenye sampuli, na wakati wa kuacha kukusanya data zaidi. Kwa kutumia mbinu hii, sampuli katika utafiti wetu ilikuwa walimu nane (8) wanaofundisha fasihi ya Kiswahili katika kidato cha tano pamoja na wanafunzi mia moja na moja (101) wanaojifunza Kiswahili na fasihi yake katika kidato cha tano kutoka shule nne zenye michepuo

ya Kiswahili. Aidha, wanafunzi kumi (10) na walimu nane (wote) ndio walifanya mahojiano. Idadi ya wanafunzi kumi ilipatikana kwa kuzingatia ufaulu wao darasani. Wale wenye ufaulu mkubwa zaidi kutokana na ripoti za shule ndio walifanya mahojiano. Hii ni kutokana na ukweli kwamba utafiti wa kitaamuli hauweki maanani kwa jinsi sampuli ya wahojiwa ilivyo au jinsi uzoefu unavyosambazwa kwa jamii nzima ya watafitiwa na hivyo kutoa fursa ya kujumuisha matokeo ya utafiti kwa jamii nzima ya watafitiwa. Aidha, lengo kuu la sampuli katika utafiti wa kitaamuli ni kutafuta watu ambao wanaweza kutoa maarifa tajiri na tofauti kuhusu jambo linalochunguzwa (Dornyei, 2007).
Sampuli ya kazi zilizoteuliwa ni hadithi fupi simulizi 4, hadithi fupi andishi 2, wimbo mmoja, shairi andishi moja na kazi nyingine mbalimbali za fasihi kama vile vitendawili, methali nahau na misemo. Kazi zilizoteuliwa zote zinapatikana katika kitabu cha Kiswahili kwa mwanafunzi wa kidato cha tano mchepuo wa Kiswahili. Kitabu hiki kimechaguliwa kwa sababu ni kitabu pekee cha mwongozo kwa somo lote la Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha tano. Walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika kidato cha tano waliteuliwa kwa kuwa ndio wanaojishughulisha na tanzu mbili za fasihi (fasihi simulizi na fasihi andishi) katika masomo yao. Hivyo basi, hawa ndio walikuwa na uwezo wa kufafanua kwa kina athari ya fasihi katika ukuzaji wa lugha yao na uwezo mbalimbali wa kimaisha.

Utafiti huu ulitumia mbinu tatu katika ukusanyaji wake wa data. Mbinu hizo ni pamoja na ushuhudiaji, uchambuzi matini na usaili (mahojiano). Katika mchakato wa ushuhudiaji, mtafiti alichunguza jinsi walimu wanavyojumuisha fasihi wakati wa ufundishaji wa lugha au wakati wa ukuzaji wa uwezo fulani miongoni mwa wanafunzi. Watafiti walishuhudia katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji darasani. Katika uchanganuzi wa matini, watafiti walichanganua matini tofauti zinazohusiana na fasihi pamoja na mtaala unaoegemea katika uwezo ili kutafuta misingi, maoni na mawazo ya wataalamu wengine juu ya suala la utafiti. Katika usaili, watafiti walihojiana na watafitiwa kuhusu mada ya utafiti. Mahojiano yalifanywa kwa lugha mbili ambazo ni lugha ya Kiswahili na Kinyarwanda. Kiswahili kilitumika kwa walimu wa Kiswahili na Kinyarwanda kikatumika kufafanua pale palipoonekana hapajaeleweka kwa sababu ya changamoto ya lugha.

Uchambuzi na uwasilishaji wa data ulitumia misimbo ili kutofautisha watafitiwa wetu wa utafiti. Kwa mfano; tulitumia A kuwakilisha shule ya kwanza, B kuwakilisha shule ya pili, C kuwakilisha shule ya tatu, D kuwakilisha shule ya nne. Katika mfumo huu, mwalimu anawakilishwa na nambari za kawaida ilhali mwanafunzi huwakilishwa na nambari za kirumi. Kwa hivyo, mwalimu wa kwanza kutoka shule ya kwanza aliitwa A1, wa pili A2, wa tatu A3 na kuendelea katika mfumo huu. Mwanafunzi wa kwanza kutoka shule ya kwanza pia aliwakilishwa na AI, wa pili AII, wa tatu AIII na kuendelea. Misimbo hii ilitumika kwa walimu na

wanafunzi wa shule zote. Kwa mfano; mwanafunzi wa nane kutoka shule ya nane aliwakilishwa na HVIII ilhali mwalimu kutoka shule hii ni H8.

**4.0 Matokeo ya Utafiti**

Data kutoka katika mapitio ya maandiko ikiwa ni pamoja na muhtasari wa kozi ya Kiswahili zimetuwezesha kubainisha mambo ya msingi yanayosisitizwa na mtaala unaoegemea katika uwezo. Hivyo basi, matokeo ya utafiti wetu ulioibua makala hii, yanawasilishwa na kujadiliwa katika sehemu kuu tatu. Matokeo ya sehemu ya kwanza yanahusu ukuzaji wa uwezo wa jumla kwa kutumia fasihi. Sehemu ya pili inahusiana na matumizi ya fasihi katika ufundishaji wa masuala mtambuka. Sehemu ya tatu inajadili ufundishaji wa mitazamo na thamani kupitia fasihi na sehemu ya mwisho inahusiana na changamoto za matumizi ya fasihi kama nyenzo ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

**4.1 Ufaafu wa Fasihi kama Nyenzo ya Kukuza Uwezo wa Jumla**

Kutokana na uchambuzi wa matini za REB (2015), CBSE (2002) na Lan (2020) uwezo wa jumla hurejelewa kwa namna tofauti: stadi zisizo za kiutambuzi, stadi laini, stadi nzima za ukuzaji mtoto, stadi zinazohamishika, stadi za maisha, stadi za kuhamasishwa, stadi za kijamii na kihisia, umilisi wa jumla na stadi za karne ya 21.

CBSE (2002), inafafanua uwezo wa jumla kama seti pana ya maarifa, ujuzi, tabia za kufanya kazi, na sifa zinazoaminika kuwa muhimu sana ili mtu aweze kuwa na mafanikio katika dunia ya sasa. Kwa kifupi, uwezo wa jumla unarejelewa kama ujuzi unaohitajika kuwezesha mtu binafsi kukabiliana na changamoto za ulimwengu wa karne ya 21.

Aidha, uwezo wa jumla unabainishwa kama uwezo wa kinyenzo, kiushirikiano, na uwezo wa kimfumo ambao unazingatia sifa za jumla na za kushirikishwa kwa kiwango chochote kile (González & Wageneer, 2003). Hii ina maana kwamba, uwezo wa jumla unajumuisha sifa za kumwezesha mtu kuishi katika kila muktadha wa kimaisha. Aidha, uwezo wa jumla ni uwezo muhimu katika nyanja mbalimbali za maisha na unachangia kwa maisha yenye mafanikio pamoja na jamii yenye ustawi (Boni & Lozano, 2007).

Hivyo basi, uwezo wa jumla unahitajika ili kuwasaidia wahitimu kuwa ni wafanyakazi wa zama za kidijiti wenye sifa zifuatazo: kuanzisha makampuni madogomadogo katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kujiajiri mwenyewe, kumiliki biashara, kubadilisha kazi kadri muda unavyopita, kuwa na werevu wa kidijiti au umilisi wa kidijiti, kutegemea sana mitandao isiyo rasmi ya kijamii ili kupata biashara (Mlaga, 2021). Katika sehemu inayofuatia tunajadili aina mbalimbali za uwezo wa jumla huku tukionesha ni kwa namna gani fasihi ni nyenzo mwafaka katika ukuzaji wa uwezo husika.

**4.1.1 Fasihi katika Ukuzaji wa Tafakuri Tunduizi**

Tung na Chang (2009) wanabainisha kuwa tafakuri tunduizi ni upataji wa uamuzi kutokana na kile kinachohitajika katika hali ya mwamuzi binafsi, mtu au kitu kingine au jamii kubwa. Wanatanabahisha kwamba fasihi ni muhimu sana katika ukuzaji wa tafakuri tuduizi kutokana na sababu zifuatazo: mosi, mchakato wa kiakili wa usomaji wa fasihi unahitaji uwezo wa tafakuri tunduizi. Hii ni kwa sababu usomaji wa fasihi ni mchakato changamano unaohitaji wasomaji kukumbuka, kurejesha na kutafakari tajriba zao za awali ili kujenga maana za matini. Pili, mada, mazingira na lugha ya kazi ya fasihi huwapa wasomaji aina mbalimbali za matukio ya ulimwengu halisi. Aidha, Abida (2016) anaeleza kwamba matumizi ya fasihi katika ufundishaji husaidia kupatikana kwa mahali mwafaka pa kuanzia kukuza tafakuri tunduizi. Kutokana na mawazo ya wataalamu hawa ni dhahiri kwamba stadi ya tafakuri tunduizi ni msingi wa uwezo mwingine wowote wa jumla. Hii ni kutokana na ukweli kuwa uwezo mwingine wote hujengeka kwenye msingi wa fikra sahihi zenye kujenga jamii na watu wake kama lengo kuu la mtaala unaoegemea katika uwezo. Hata hivyo, wataalamu hao hawakueleza nafasi ya fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

Data za ushuhudiaji nazo zinathibitisha madai kwamba fasihi inachangia sana kukuza tafakuri tunduizi. Ila, walimu wanafundisha fasihi kama somo tu yaani hawaitumii kama nyenzo ya kuwasaidia kukuza tafakuri tunduizi na stadi nyingine za karne ya ishirini na moja miongoni mwa wanafunzi. Hii ni kwa sababu walimu wote walifundisha fasihi pasipo kufundisha mada nyingine kwa kutumia fasihi. Hata hivyo, katika madarasa yaliyokuwa yakishughulikia kazi za fasihi, wanafunzi walikuwa wakivutiwa na hadithi pamoja na riwaya. Mvuto huo uliwafanya kushiriki vema katika kutoa maoni kuhusiana na kazi zinazoshughulikiwa. Ushiriki hai ulijitokeza zaidi katika utoaji wa hitimisho au utoaji wa mapendekezo juu ya mwisho wa kazi zinazoshughulikiwa, uendelezaji wa visa na matukio, na utoaji wa suluhisho la migogoro baina ya wahusika. Hali hii ilikuwa tofauti katika madarasa yaliyokuwa yanashughulikia sarufi na mada nyinginezo bila utumiaji wa fasihi. Katika madarasa yasiyotumia fasihi, ilionekana kukosekana kwa ushiriki hai kwa upande wa wanafunzi.

Nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi unadhihirishwa pia na maoni ya walimu. Kwa mfano, mwalimu CH1 anasema:

> "…wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi wanafunzi hufikiri zaidi. Mimi nafurahi wakati tunapojifunza hadithi inayoeleweka kwa wanafunzi kwa sababu wanaleta mawazo mapya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Wakati wanapoelewa kazi inayoshughulikiwa wanajibu kila swali linaloulizwa kuhusu kazi hiyo. Ingawa siyo rahisi kupata kazi ya fasihi inayolingana na viwango vyote vya wanafunzi, lakini

> wanapoielewa kazi husika wanaweza kutoa utatuzi sahihi wa migogoro kati ya wahusika au kutoa mwisho wenye manufaa kwa jamii lengwa".

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Dondoo hili linatuonesha kwamba walimu wanasubiri kufanikiwa kwa ajili ya fasihi wakati wa mada za fasihi ila hawafundishi mada nyingine kwa kutumia fasihi kama nyenzo. Kutokana na dondoo la hapo juu, utumizi wa kazi mwafaka ya fasihi kwa mwanafunzi huwa ufunguo wa kutafakari na kujenga mawazo yenye manufaa kwake na kwa jamii. Hali hii huwa mojawapo ya sababu za kuifanya fasihi kuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.
Matokeo haya yalipatikana kutokana na msingi wa Nadharia ya Mwingiliano wa Tamaduni-jamii unaodai kwamba ushirikishwaji wa ujuzi si manufaa ya mtu binafsi tu bali pia jamii pana. Kwa hivyo, fikra nzuri kutokana na uhakiki wa kazi za fasihi huchangia sana katika maendeleo ya jamii husika kama lengo la mtaala unaoegemea uwezo. Kwa maneno mengine nadharia hii ilitusaidia kuoanisha ujuzi unaotokana na kazi za fasihi na mahitaji ya mtaala unaoegemea uwezo. Uhusiano uliopo ndio ulitufanya kuwa na wazo la kwamba fasihi inaweza kuwa nyenzo mwafaka ya kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo na kufanya utafiti ulioibua makala hii.

### 4.1.2 Fasihi na Ukuzaji wa Utafiti na Utatuzi wa Tatizo

Kwa mujibu wa Shute na wenzake (2016), utatuzi wa tatizo unahusiana na hatua za kupanga njia za suluhisho la tatizo kwa kutumia zana na rasilimali kwa ufanisi na huku kukiwa na ufuatiliaji wa maendeleo ya utatuzi wa tatizo husika. Utafiti ni ukusanyaji wa taarifa juu ya tatizo fulani, kukagua taarifa hizo, kuzichambua na kuzifasili kwa namna ambayo huleta suluhisho la tatizo. Hivyo basi, utafiti nao unahusu kutafuta jibu la tatizo lililopo. Hivyo, utafiti tunaweza kuutazama kama juhudi na harakati za kutengeneza na kupata maarifa mapya.

Uhusiano wa fasihi, utafiti, na utatuzi wa tatizo unabainishwa na baadhi ya wataalamu kama vile Huda na Bushra (2021). Wataalamu hawa wanaeleza kuwa uchambuzi wa matini za kifasihi, huwawezesha wanafunzi kufanya tathmini, kuainisha na kisha kuunganisha maudhui yanayotolewa na maandiko ili kukuza stadi ya kutatua matatizo yanayowakabili wahusika. Aidha, data kutoka mahojiano zinathibitisha mawazo ya wataalamu hawa. Lifuatalo ni dondoo la mwanafunzi BIII akieleza jinsi fasihi huchangia katika ukuzaji wa stadi ya utafiti na utatuzi wa matatizo:

> "…wakati tunaposoma kazi za fasihi mara nyingi tunalenga kuelewa maana ya mtunzi. Hali hii inatusaidia kupata maana yenyewe ambayo mtunzi anataka itufikie kama hadhira yake. Katika mchakato huu, tunajifunza mengi kutokana na kazi yote

aghalabu kutokana na wahusika. Kwa mfano: katika hadithi ya Nyambere, tuliona kwamba Mariya alikuwa anamchukia sana nduguye Nyambere. Wakati huu, Nyambere aliongeza upendo kwake kwa kiasi cha Maria naye kumpenda. Hali hii iliwafanya kushirikiana ili walitoroke zimwi".

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Dondoo hili, linatuonesha namna ambavyo fasihi hujumuisha mifano halisi ya matatizo yaliyopo katika jamii. Aidha, tunaelezwa pia namna ambayo fasihi huibua fikra za wanafunzi katika kukabili matatizo wanayoweza kukutana nayo katika maisha halisi. Wakati wa ushuhudiaji darasani, wanafunzi na mwalimu walikuwa wanashughulikia hadithi fupi iitwayo 'Nyambere na Maria'. Kutokana na hadithi hii wanafunzi wa shule B walipata suluhisho la tatizo la ugomvi na chuki miongoni mwa ndugu na hata wanajamii kwa jumla. Suluhisho hilo lilikuwa kuwapenda watu wote hata wale wanaowachukia. Bila shaka, mkakati huu ukitekelezwa katika maisha yao halisi, litakuwa suluhisho la tatizo linalokabili jamii na familia nyingi duniani. Tatizo hili la ugomvi na chuki miongoni mwa watu, huleta vita na kutatiza maendeleo hasa ya kiuchumi. Hivyo basi, wahitimu wa shule husika, waliamua kutafuta amani, mshikamano na upendo katika jamii zao kama miongoni mwa malengo ya mtaala unaoegemea uwezo.

### 4.1.3 Fasihi kama Nyenzo ya Ukuzaji wa Ubunifu na Ugunduzi

Binadamu anatarajiwa kuwa mbunifu na mgunduzi katika maisha yake yote. Hata hivyo, wanadamu wa leo wako katika enzi mpya ambapo mawazo ya ubunifu yanahitajika kwa kiasi kikubwa kuliko enzi zilizopita (Nakano & Wechsler, 2018). Aidha, Nosratinia & Zaker (2014) wanaeleza kuwa uwezo wa ubunifu na ugunduzi huweza kukuzwa kupitia fasihi kutokana na utumizi wa mikakati tofauti. Mikakati hii ni kama vile kutafakari juu ya kazi husika ya fasihi, uorodheshaji wa maswali kuhusu kazi husika, na ubadilishaji wa sifa za wahusika, maswali ya msomaji, maswali ya mitihani ya wanafunzi, na kuisimulia hadithi kwa upya tukitaja kwa uchache.

Hata hivyo, data za ushuhudiaji zilituonesha kuwa walimu wanafundisha fasihi kama somo ila hawaitumii kama nyenzo ya kukuza uwezo wa ubunifu na ugunduzi miongoni mwa wanafunzi. Ila wakati wa kushughulikia mada za kifasihi, wanafunzi hufikiria sana na kuoanisha mawazo ya kila mhusika ili kutafuta suluhisho la migogoro lililopo kati yao. Hatuna budi kusema kuwa ujuzi huu wanaoupata darasani unaendelea kutumiwa katika michakato ya utatuzi wa matatizo katika jamii zao halisi. Hata hivyo, wakati wa mahojiano maoni ya walimu yalitetea wazo la kwamba fasihi inazingatia mifano ya ugunduzi na uvumbuzi kama asemavyo mwalimu D1:

> "Mara nyingi fasihi simulizi ya Afrika hutumia Sungura kama mnyama mwenye ubunifu na ugunduzi sana. Uwezo huu mara nyingi humwokoa kutoka katika majanga kadhaa na wakati mwingine anautumia kuokoa wahusika wengine. Vitendawili na mafumbo nayo huwahamasisha wanafunzi kufikiria mbali kwa kutumia busara ili kuleta kitu kipya chenye manufaa binafsi na kwa jamii kwa jumla".
>
> **Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Dondoo la hapo juu linadokeza kwamba fasihi huwaongoza na kuwafundisha wanafunzi kutochukua uamuzi kiholela holela juu ya suala au tatizo fulani linalopaswa kutafutiwa suluhisho katika maisha yao ya kila siku. Zaidi ya hivyo, kazi za fasihi huwahamasisha wanafunzi kufikiria kwa kina ili kuleta upya. Upya huu unaweza kuwa wa wazo, tendo au kitu chenye manufaa kwao binafsi, na kwa wanajamii kwa ujumla. Aidha, tunatambua kwamba fasihi ikitumiwa kukuza ubunifu na ugunduzi, wanafunzi watajengewa mazingira mazuri yanayohusiana moja kwa moja na hali halisi ya maisha. Hivyo basi, kwa upande wa ufundishaji wa Kiswahi, fasihi inapaswa kutumika kama njia siyo tu ya kutoa kanuni mbalimbali za sarufi, sintaksia na fonolojia lakini pia kuboresha ubunifu wa wanafunzi.

### 4.1.4 Fasihi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano

Stadi za mawasiliano zinahusu uwezo wa mtu kujumuisha na kutumia ujuzi mbalimbali ili kila mtu anayehusika na mawasiliano hayo aweze kuelewa (Wambui, 2016). Ujuzi huu ni pamoja na kufikiria la kusema, kutafuta njia bora ya kulisema, kutafuta maneno sahihi, kumuelewa mtu au watu ambao mnawasiliana, na kuzingatia muktadha wa mawasiliano. Al Odhayani na Ratnapalan (2016) wanabainisha njia za kukuza stadi za mawasiliano kama zifuatazo: kuiga kutoka kwa mwalimu, kutazama videwo zenye sauti, kutumia michezo ya kuigiza, kutumia makundi ya mijadala, na kuiga wazazi, kutumia sauti za kielektroniki. Matumizi ya mijadala, michezo ya kuigiza na nyenzo za TEHAMA husisitizwa hata katika mtaala unaoegemea katika uwezo.

Matokeo ya utafiti uliozalisha makala hii, yanatanabahisha kwamba fasihi hujumuisha stadi za mawasiliano. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wakati wa ujishughulishaji wa kazi za fasihi, wanafunzi waliwasilisha maoni tofauti juu ya tabia za wahusika, mihtasari ya kazi zinazoshughulikiwa pamoja na uwezekano wa yanayofuata baada ya sehemu fulani au mwisho wa hadithi husika. Hivyo, kuifanya fasihi kuwa nyenzo mwafaka ya ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za mawasiliano. Kupitia fasihi, wanafunzi walikuwa wakiiga stadi za mawasiliano zinazodhihirishwa na wahusika wa kazi za fasihi. Hata katika mahojiano, wanafunzi

walilitetea jambo hili na wanapendekeza fasihi itumiwe kuwakuzia uwezo huu. Kwa mfano, mwanafunzi AIII anasema:

> "…Baadhi ya kazi za fasihi zinatufundisha ujuzi tofauti wa kuwasiliana na watu tofauti kulingana na umri wao kama vile wazee, vijana, watoto, wazazi na kadhalika. Pia, zinajumuisha mawasiliano katika miktadha mbalimbali kama vile kanisani, darasani, msibani, nyumbani, mezani na kadhalika. Kwa hivyo, ni vizuri kusoma au kusimuliwa hadithi ili nawe uitolee maoni yako".

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Maoni kutoka baadhi ya watafitiwa kama yanavyobainishwa hapo juu, yanaonesha kuwa fasihi hujumuisha mifano ya matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. Kwa hivyo, kutokana na fasihi, wanafunzi wanaweza kuhamisha ujuzi kutoka kazi za fasihi na kuutekeleza katika mawasiliano yao halisi.

Aidha, kutokana na ulimwengu wa kisasa ambao unasisitiza mawasiliano ya kiteknolojia, mawasiliano hubadilishwa sana na teknolojia mpya. Kwa hivyo, mawasiliano yanayosisitizwa katika miktadha ya kiuchumi yanapaswa kuzingatia matumizi ya vifaa kama vile simu, redio, televisheni, filamu, uchapishaji, barua za kielektroniki, mikutano ya videwo na teknolojia ya mtandao kwa jumla. Fasihi nayo haipuuzi kipengele cha teknolojia kulingana na maendeleo ya jamii. Hoja hii inathibitishwa hata na walimu tuliowahoji. Kwa mfano, mwalimu C1 anabainisha kuwa:

> '…leo, hadhira kubwa ya fasihi hasa ya fasihi andishi hupatikana kwenye mitandao. Hii ni tofauti na zamani ambapo uwasilishaji ulikuwa kupitia kalamu na watu wa karibu yake. Aidha, tunaona michezo ya kuigiza, tunasikiliza au kutazama tamthilia na komedi kupitia mitandao na televisheni au redio. Hayo ni mabadiliko ya fasihi kulingana na hali ya kijamii'.

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Dondoo hili linatanabahisha kwamba fasihi inatoa mifano ya utunzi wa kisasa ambao unastahili kufundishwa wanafunzi ili waweze kuutekeleza mahitaji ya maisha halisi ya ulimwengu wa kisasa. Aidha, ni dhahiri kwamba shughuli zote za kimaisha na kiuchumi huweza kufundishwa kupitia fasihi.

### 4.1.5 Ushirikiano na Utawala Binafsi

Matos na Afsarmanesh (2008) wanafafanua jinsi ushirikiano unavyojumuisha habari, rasilimali na majukumu. Kutokana na hali hii, tunaona kuwa maisha

hayawezi kufanikishwa bila ushirikiano. Hata hivyo, ushirikiano unawezekana kati ya viumbe vyenye malengo sawa kuhusu ushirikiano husika. Aidha, Jyotsna na Dwarakanath (2018) wanabainisha kwamba, fasihi inafaa sana kufahamisha, kushawishi, kumotisha na kuvutia akili changa. Ni dhahiri kwamba wataalamu hawa wanamaanisha kuwa fasihi inaweza kutumiwa kumbadilishia na kumfanya mtu arekebishe tabia fulani. Hali hii bila shaka, inahusiana na ukuzaji wa stadi za maisha.

Aidha, data za ushuhudiaji zilituthibitishia kwamba kupitia kazi za fasihi kama vile hadithi wanafunzi wamepata mafundisho na mifano ya kuimarisha ushirikiano na utawala binafsi miongoni mwao na jamii. Kwa mfano, katika darasa D walikuwa wakishughulikia hadithi moja simulizi ambapo ndugu wa kike wawili walikuwa wanachukiana. Aidha, mmoja aligundua kwamba nduguye aliolewa na zimwi. Kwa hivyo, yule asiyeolewa aliamua kumshauri nduguye na kumshawishi kwamba aliolewa na zimwi na wakapanga kulitoroka moja kwa moja. Siku hiyo walipambana kwa pamoja wakafanikiwa katika vita vikali na zimwi hilo. Kutokana na hadithi hii, wanafunzi walijifunza umuhimu wa ushirikiano pamoja na mchango wa kila mtu katika utawala wake binafsi.

### 3.1.6 Fasihi kama Nyenzo ya Ukuzaji wa Ujifunzaji wa Kudumu

Ujifunzaji wa kudumu ni ujifunzaji unaojitokeza katika maisha yote ya mtu tangu kuzaliwa hadi kufa (Kaplan, 2016). Kutokana na umuhimu wake, ujifunzaji wa kudumu unapaswa kukuzwa kwa kujielekeza katika kuzingatia miktadha mbalimbali ya maisha. Mwanafunzi anapaswa kuelewa kwamba, maisha yote yametawaliwa na michakato ya ujifunzaji. Hii ina maana kwamba, hata baada ya mwanafunzi kuhitimu shule, bado atalazimika kujifunza kutokana na mabadiliko mbalimbali yanayojitokeza katika jamii na ulimwengu wake halisi.

Data zilizotokana na ushuhudiaji zilionesha kwamba wanafunzi wanapenda kuhakiki tabia za wahusika mbalimbali kutoka kazi za fasihi. Wakati huu wa ushuhudiaji wanafunzi walikuwa na hamu ya kuzua mijadala juu ya ujuzi wa kila mhusika na kujifunza kutokana naye hususani katika utatuzi wa matatizo, ubunifu, tafakari na uwezo mwingine ambao mtu anaweza kutumia katika maisha yake halisi. Aidha, madarasa mawili katika madarasa manne yaliyoshuhudiwa yalikuwa yakishughulikia mazungumzo na vifungu vya habari visivyo vya kifasihi. Hata hivyo, tumebainisha kuwa mazungumzo na vifungu vya habari vingine havijumuishi miktadha na mifano halisi inayofaa kukuza ujifunzaji wa kudumu inavyofanya fasihi.

Hata data zilizotokana na usaili ziliteteа kuwa ujifunzaji wa kudumu unafaa kukuzwa kupitia fasihi. Hili ni mojawapo ya madondoo kutoka kwa wanafunzi walipoulizwa jinsi ambavyo fasihi inaweza kukuza uwezo huo. Mwanafunzi AV alisema:

> "Wakati tunapohakiki kazi za fasihi katika makundi, tunashirikishana mawazo. Kwa hivyo, mwanafunzi huweza kujifunza kutoka kwa mwenzake. Zaidi ya hayo, kazi nyingi za fasihi humalizika kwa mhusika mbaya kubadilika. Hali hii hutufanya kubadilisha fikra zetu kuelekea mahitaji ya jamii pana".

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Dondoo hili linabainisha jinsi ambavyo wanafunzi wanaamini kwamba fasihi hujumuisha mifano na mafunzo juu ya ujifunzaji wa kudumu. Hata hivyo, jambo la muhimu zaidi ni kwamba fasihi huhamasisha tabia ya kujifunza kutoka kwa wanarika, jamii, pamoja na kutoka kwa watu mbalimbali. Fasihi pia husisitiza hali ya kukubali makosa yaliyofanywa na kukubali kuyakosoa. Hali hii huwafanya wanafunzi kupata maarifa mapya ambayo huwawezesha kujifunza wakati wote. Aidha, fasihi hutoa mifano mwafaka ya wahusika ambao ni mifano bora ya watu walionufaika kutokana na ujifunzaji wa kudumu.

### 4.2 Fasihi kama Nyezo ya Ufundishaji wa Masuala Mtambuka

Kwa upande wa masuala mtambuka, mihtasari ya masomo nchini Rwanda inabainisha masuala mtambuka kuwa ni pamoja na ujasiriamali, elimu ya afya ya uzazi na UKIMWI, utunzaji wa mazingira, maendeleo endelevu, umoja na maridhiano, mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi, tukitaja kwa uchache (REB, 2015). Hivyo basi, tunaona ni muhimu kujadili nafasi ya fasihi katika kufanikisha ufundishaji wa masuala mtambuka yanayobainishwa na mtaala unaoegemea katika uwezo kupitia mihtasari na silabasi zake.

Kutokana na hali iliyopo sasa, serikali inapambana na changamoto mbalimbali kama vile watoto wa mitaani, janga la UKIMWI, mimba za utotoni, ujasiriamali, na utunzaji na uhifadhi wa mazingira tukitaja kwa uchache. Kutokana na fasili ya masuala mtambuka, tunatambua kwamba masuala mtambuka hujumuisha masuala yanayojitokeza katika maisha ya kila siku ya wanajamii. Hivyo, nyenzo zinazotumiwa kufundishia masomo mengine zinapaswa kujumuisha vema masuala mtambuka. Aidha, ni lazima mtu awe na uelewa wa kutosha kuhusu masuala mtambuka katika maisha yake ya kila siku. Hata hivyo, kuna kazi nyingi za kifasihi zinazofafanua na kueleza masuala mtambuka mbalimbali. Kutokana na hali hii, makala inabainisha ufaafu wa fashi katika ujumuishaji na ufafanuzi wa baadhi ya masuala mtambuka.

#### 4.2.1 Fasihi na Ujasiriamali

Katika karne ya 21, ujasiriamali hufungua fursa kwa watu. Fursa hiyo inahusu kuelewa upya njia za kudhibiti biashara kutoka kwa mtazamo wa kimataifa pamoja na jinsi ya kutumia teknolojia ambayo hutawala shughuli za binadamu wa kisasa

(Sampene na wenzake, 2021). Hivyo basi, ujasiriamali unaonekana kuwa na mchango mkubwa katika maisha na maendeleo ya mtu wa kisasa. Walimu wanaonekana wanakubaliana kuwa fasihi ni nyenzo muhimu ya kufundisha ujasiriamali. Hii ni kwa sababu kazi za fasihi hujumuisha mifano ya kufundisha ujasiriamali miongoni mwa wanafunzi. Mwalimu B1 anathibitisha hili anaposema:

> "Kuna baadhi ya kazi za fasihi zinazotumia lugha au wahusika wanaohusiana na ujasiriamali. Kwa mfano, riwaya ya *Adili na Nduguze* iliyoandikwa na Shaaban Robert mwaka 1952 huzungumza biashara na ujasiriamali katika njia tofauti. Kwa njia ya kwanza, *Adili na nduguze* walikuwa watu wenye hamu ya ujasiriamali. Kuna matumizi ya methali kama "mali bila daftari hupotea bila habari"

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Kutokana na dondoo la mwalimu B1, tunaelezwa kuhusu mfano wa ujasiriamali ujumuishwayo katika wa riwaya ya *Adili na Nduguze*. Kwa hivyo, tunatambua kwamba katika riwaya hii Robert (khj) alitaka kuwafundisha watu shughuli za kibiashara na ujasiriamali. Adili alikuwa makini sana katika shughuli za kibiashara. Hata methali aliyotumia "Mali bila daftari hupotea bila habari" inaweka wazi wazo la kwamba mafanikio ya biashara ni kuhifadhi taarifa za biashara. Zaidi ya hayo, katika riwaya ya *Adili na nduguze* mtunzi anaonya watu kwamba uhifadhi bora ni ule wa kimaandishi. Hii ni kwa sababu maandishi huendelea kurejelewa na hayasahauliki kama maneno. Kwa hivyo, ni rahisi kufundisha masuala yanayohusiana na biashara au ujasiriamali kupitia kazi mbalimbali za fasihi.

### 4.2.2 Fasihi na Usawa wa Kijinsia

Usawa wa jinsia unachangia sana katika maisha ya ulimwengu wa kisasa. Umesababisha maendeleo katika kila nyanja za maisha. Hii ni kwa sababu majukumu ya mwanamke wa kisasa hayaishii tena kwa kupika, kuosha vyombo, kufanya kazi za nyumbani, na kutunza watoto. Zaidi ya hayo, mwanamke sasa hufanya kazi mbalimbali za kimaendeleo kama afanyavyo mwanaume.

Hata hivyo, Mlaga (2017) anabainisha kwamba kazi ya fasihi yenye kusawiri uzoefu wa mwanafunzi wa kike hufaa sana kumfundisha. Zaidi ya hayo, fasihi huweza kubeba taswira na ujumbe wa kupendeza kwa mwanafunzi wa kike. Hali hii humpa motisha na kumhimiza kufahamu kwa ukamilifu nafasi yake katika kuleta maendeleo kwa jamii yake. Katika utafiti wetu, data za usaili zimebainisha kwamba walimu wanaitazama fasihi kama nyenzo muhimu katika kufundisha usawa wa kijinsia na masuala mengine ya kijinsia. Kwa mfano, mwalimu C1 anasema:

> "Katika tamthilia nyingi tunakuta mambo mengi yanayojadili usawa wa jinsia. Kwa mfano, katika tamthilia ya "*Kilio cha Haki*"

> iliyoandikwa na Mazrui mnamo mwaka wa 1981 kuna wahusika wanaosawiri usawa wa kijinsia. Ila si rahisi mwanafunzi kuelewa mambo hayo kwa ajili ya ujuzi mdogo katika uhakiki".
>
> **Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Katika dondoo hili, mwalimu C1 alitumia mfano mzuri wa tamthilia inayoweza kumsaidia mwalimu kufafanua suala la usawa wa kijinsia na athari zake katika maendeleo ya jamii. Kutokana na dondoo hili, tunatambua kwamba upungufu katika matumizi ya fasihi kama nyenzo ya kufundishia masuala mtambuka upo kwa upande wa walimu. Hii ni kwa sababu walimu wangali na tabia ya kutowaamini wanafunzi wao kuwa nao wanaukomavu wa fikra kiasi cha kupambanua mambo mbalimbali.

### 4.2.3 Fasihi na Elimu ya Afya ya Uzazi na UKIMWI

Elimu kuhusu afya ya uzazi na UKIMWI inahitajika kukuzwa sana miongoni mwa wanafunzi kama inavyosisitizwa na mtaala unaoegemea uwezo. Hii ni kutokana na umuhimu wake wa kusaidia watu kuepukana na magonjwa ya kuambukizwa ambayo yanatesa maisha ya watu wa leo (Croce-Galis na wenzake, 2014).

Kutokana na data za ushuhudiaji, tuliona kwamba walimu na wanafunzi wanashughulikia kazi za fasihi ambazo huweza kuwasaidia kufundisha suala hili kwa urahisi. Ila, tatizo ni kwamba walimu hushindwa kuoanisha ujumbe uliopo na elimu kuhusu afya ya uzazi na UKIMWI. Kwa mfano kuna madarasa yaliyokuwa yakishughulikia methali na nahau kama vile

1. Afya ni kama maji yakimwagika hayazoleki
2. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu, na
3. Maradhi yaingiavyo, sivyo yatokavyo'.

Walimu hawakulinganisha methali hizi na suala la elimu kuhusu afya ya uzazi na UKIMWI ingawa ilikuwa fursa ya kufundisha suala hili kutokana na methali hizi. Hii ni kwa sababu kutokana na methali ya kwanza kuna maonyo kwa wanafunzi kwamba wakiambukizwa magonjwa kama UKIMWI, afya na maisha yao hayatarudia katika hali nzuri kamwe. Kuhusiana na methali ya pili, mwalimu angeweza kuwashawishi wanafunzi kutii maonyo ya wazazi na walezi wao hususani kuhusiana na afya ya uzazi. Hapa ni bora kusisitiza umuhimu wa malezi ya wazazi na walezi wa wanafunzi kuhusu suala hili. Katika usaili, walimu walibainisha namna ambavyo fasihi inaweza kujumuisha suala la elimu ya afya ya uzazi na UKIMWI. Kwa mfano, mwalimu A2 anatanabahisha kuwa:

> "Kuna mashairi, misemo, methali nyingi zinazojadili suala la elimu ya afya ya uzazi na UKIMWI. Nyimbo nyingi za Wanyarwanda wa leo zinazungumza sana masuala haya kama vile mimba za utotoni, maambukizi ya UKIMWI, na hata kuzaa watoto wengi pasipo uwezo wa kuwalea ipasavyo tukitaja kwa uchache".

> **Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Dondoo hili, linatuangazia kwamba baadhi ya walimu wametambua kuwa fasihi inajumuisha na kutoa mifano ya kufundishia elimu ya afya ya uzazi na UKIMWI. Ila, tatizo ni kwamba wanashindwa kuzihusianisha kazi za fasihi na ufundishaji wa suala hili. Wakati wa mahojiano pia tulipewa ushahidi kwamba hata wanafunzi wanapopewa fursa wanajitungia kazi za kufundishia na kujifunza kuhusu afya ya uzazi na UKIMWI. Dondoo lifuatalo linatoa taarifa zaidi:

> Mimi nina shairi ambalo nilitunga wakati wa mashindano yaliyoandaliwa na HDI kuelekea siku ya UKIMWI duniani. Shairi langu lilikuwa hasa linatoa maonyo kwa vijana kuhusu namna ya kujikinga na maradhi haya. Aidha, lilikuwa linaeleza maana ya UKIMWI, jinsi unavyosambazwa na namna ya kujiepusha na maradhi haya na kuyazuia miongoni mwetu. Siku hiyo, shairi langu lilipata nafasi ya kwanza katika wilaya yetu.
>
> **Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Kutokana na uzoefu wa mwanafunzi huyu, tunatoa shime kwa walimu kutumia kazi za fasihi zilizotungwa na wanafunzi wenyewe kufundisha masuala mtambuka. Tunaporejea mtaala unaoegemea katika uwezo, hali ya kutumia kazi zilizotungwa na wanafunzi wenyewe ni mbinu nzuri na inayohitajika katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo. Hivyo basi, kutokana na madondoo hayo, fasihi inafaa kutumiwa kama nyenzo ya kufundishia elimu ya afya ya uzazi na UKIMWI.

### 4.2.4 Fasihi na Elimu kuhusu Utunzaji wa Mazingira na Uhifadhi

Mkakati wa utunzaji wa mazingira ni mwongozo muhimu katika kuleta maendeleo endelevu na kupunguza umasikini (Assey na wenzake, 2007). Utunzaji wa mazingira na uhifadhi ni mambo muhimu sana katika maendeleo endelevu ya mtu na jamii kwa jumla. Hii ndiyo sababu suala hili linatiliwa nguvu sana katika zama za sasa.

Kutokana na data za ushuhudiaji tuliona kuwa walimu na wanafunzi wanashughulikia kazi za fasihi zenye mifano ya kufundishia suala la utunzaji wa mazingira na uhifadhi ila walimu wanashindwa kutumia fursa hii kufundishia. Katika darasa la kidato cha tano kutoka shule B walikuwa wanashughulikia riwaya ya *Adili na Nduguze*. Katika riwaya hii tunaona uzuri na umuhimu wa mazingira kama vile mawe, majohari, maji, milima, wanyama kama ndege tukitaja kwa uchache. Hata katika data za mahojiano walimu walionesha kuwa wanaelewa kwamba fasihi inazingatia mifano ya ufundishaji wa utunzaji wa mazingira na uhifadhi. Mwalimu B2 anathibitisha hili kwa kusema:

> "Kuna kazi za fasihi zinazoeleza suala la utunzaji wa mazingira na umuhimu wake. Kwa mfano: riwaya ya *Adili na Nduguze* ya Shaban Robert inaeleza namna makomamanga yalivyokuwa chakula cha Mwelekevu katika mji wa mawe. Riwaya hii inaeleza umuhimu wa madini, miti, maji, mifugo, mimea, na majabali".

**Chanzo:** Data za uwandani (2022).

Kupitia riwaya iliyotumiwa katika dondoo la hapo juu, tunaelezwa pia namna mfalme Rai alivyosisitiza utunzaji wa mazingira na uhifadhi katika nchi yake. Kutokana na hali hiyo, nchi ya Ughaibu ilifanikiwa pia katika ufugaji wa mifugo. Aidha, riwaya inaonesha pia umuhimu wa maji, majabali kama makazi ya viumbe wengine. Riwaya hii inabainisha pia umuhimu wa miti kama malighafi. Hivyo basi, riwaya hii inaweza kusaidia wanafunzi kufafanua suala la utunzaji wa mazingira na uhifadhi.

Kwa kuhitimisha sehemu ya masuala mtambuka, tunaweza kubainisha kwamba fasihi inajumuisha mifano halisi ya masuala mtambuka. Kwa hivyo, ni kazi ya walimu kuchagua kazi zinazofaa kufundisha kipengele hiki cha mtaala unaoegemea katika uwezo. Ikumbukwe kwamba uchaguzi wa kazi mwafaka za fasihi ni lazima uzingatie malengo ya ujifunzaji na kiwango cha wanafunzi.

### 4.3 Ufundishaji wa Mitazamo na Thamani kupitia Fasihi

Kwa upande wa mitazamo na thamani, muhtasari unabainisha mitazamo na thamani faafu ambayo mwanafunzi Mnyarwanda anastahili kujengewa. Mitazamo na thamani hizo ni pamoja na kupenda kazi, kufanya kazi kwa bidii na ufanisi, kuipenda nchi yake, kujitolea, kuwa mkweli, uadilifu, kusaidia wengine, kuchukia rushwa, kuepuka ugomvi walau tukitaja kwa uchache (REB 2015). Pamoja na haya, tunatambua kuwa silabasi za masomo mbalimbali ikiwa pamoja na zile za Kiswahili hazijabainisha kwa ukamilifu mitazamo yote na thamani zote muhimu zinazopaswa kupandikizwa miongoni mwa wanafunzi. Miongoni mwa mitazamo na thamani ambazo hazijatajwa katika silabasi za Kiswahili ni pamoja na utayari wa kusamehe, uaminifu, wema, ukarimu, ujasiri, na kujiamini tukitaja kwa machache. Hii itoshe kuonesha kwamba, mwalimu yupo huru kufundisha mitazamo na thamani zaidi ya zinazotajwa katika silabasi. Jambo la muhimu ni kuhakikisha mitazamo na thamani zinazosisitizwa ni zile zinazoendana na mila na desturi za Wanyarwanda au zile za raia wa kidunia.

Lekawael & Rafli (2018) wanatanabahisha kuwa fasihi ni nyenzo mwafaka ya kufundisha mitazamo na thamani. Watafiti hawa walifanya utafiti kuhusu ufundishaji wa maadili kupitia fasihi katika shule moja nchini Indonesia. Matokeo ya utafiti wao yanabainisha kwamba maandishi ya kifasihi yaliyomo katika vitabu teule vya wanafunzi, yanazingatia mitazamo na thamani za jamii ya wanafunzi lengwa. Mitazamo na thamani vilivyopatikana katika maandishi hayo, vilikuwa

heshima, uaminifu, nidhamu, usawa, kukubali ubinafsi na tofauti, kufanya kazi kwa bidii, ukarimu, ubunifu, uzuri, usawa, roho ya mapambano, kusaidiana, kujali, kujivunia, kujitegemea, na imani. Kutokana na utafiti wa Lekawael & Rafli (khj) tunaangaziwa kwamba kazi za fasihi hubeba mifano ya mitazamo na thamani za watu walengwa wa fasihi hiyo. Hivyo basi, kazi za kutumiwa katika vitabu vya kufundishia Wanyarwanda, zinapaswa kujumuisha na kuzingatia thamani na mitazamo ya Wanyarwanda.

Data za usaili zilizokusanywa zinabainisha kwamba kazi za fasihi zinazotumiwa kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi teule, hubeba mifano ya mitazamo na thamani za Wanyarwanda. Mwalimu D2 alifafanua suala hili alipoulizwa jinsi gani fasihi huweza kutumiwa kwa kufundisha maadili na mitazamo na thamani:

> "Wanafunzi wanaweza kupata mifano ya mitazamo na thamani wakati wa kujifunza fasihi. kwa mfano: riwaya ya *Adili na Nduguze* inatuonesha jinsi Ikibali alivyokuwa mwaminifu. Adili naye alikuwa mchapakazi na alikuwa na mitazamo na thamani za kusaidia watu wengine. Wananchi wa nchi ya Ughaibu nao walikuwa na thamani ya kupenda nchi yao kwa kulipa kodi vizuri, kuheshimu viumbe vyote, na kufanya kazi ya kulima na kufuga".
>
> **Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Dondoo la mwalimu B1 linatuangazia kwamba hata katika muhtasari wa Kiswahili kwa kidato teule kuna baadhi ya kazi za fasihi zinazobeba mifano ya mitazamo na thamani za Wanyarwanda. Mwalimu huyu ametoa baadhi ya mifano hiyo kama inavyojumuishwa katika mfano wa riwaya moja inayofundishwa katika darasa teule. Hata hivyo, changamoto iliyopo ni walimu kuamini tu kwamba wanafunzi watajifunza mitazamo na thamani wakati mwalimu anapofundisha fasihi kwa ujumla badala ya kuitumia fasihi kwa makusudi kama nyenzo ya ufundishaji wa mitazamo na thamani.

## 5.0 Changamoto za Matumizi ya Fasihi Kutekelezaji Mtaala Unaoegemea katika Uwezo

Baadhi ya walimu wanaofundisha fasihi wanakabiliwa na changamoto ya kuitazama fasihi kama somo tu. Walimu hawa wanasahau kuwa fasihi ina thamani yake katika kujumuisha stadi na ujuzi wa aina tofauti unaohitajika katika karne ya 21. Kwa hivyo, ni bora mwalimu asijikite tu kueleza usuli wa kazi ya fasihi husika bali anapaswa kuhakikisha kuwa wanafunzi wanafundishwa pia kuhusu jamii ya kazi ya kifasihi na kuilinganisha na jamii ya wanafunzi. Jambo hili litawasaidia wanafunzi kujenga mawazo yao, kuelewa jadi, hatua na matarajio ya jamii yao kutokana na kazi ya fasihi inayoshughulikiwa.

Ili kuhimiza ukuaji wa uwezo wa jumla miongoni mwa wanafunzi, walimu wanatarajiwa kufanya mambo yafuatayo: Mosi, kujua aina mbalimbali za kazi za fasihi na kujua juu ya urahisi na ugumu wake. Pili, walimu wanapaswa kujua kiwango cha wanafunzi wao. Kutokana na hali hii, walimu wanaweza kuchagua kazi za fasihi zinazoeleweka kwa wanafunzi wao. Tatu, walimu wanapaswa kuchagua kazi za fasihi ambazo zinaweza kuhusishwa na hali halisi ya maisha ya wanafunzi ili ziweze kuwa mifano mwafaka ya ufundishaji wa utamaduni, masuala ya jamii halisi na mitazamo na thamani za wanafunzi na Wanyarwanda kwa jumla.

Changamoto ya mwisho inahusiana na uhaba wa kazi za fasihi (Bhaskar, na wenzake 2017). Ili kuepukana na tatizo hili, tunatoa rai kwa wataalamu wa fasihi kuongeza jitihada za kuandika vitabu vya fasihi (mashairi, riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ngonjera) kwa wingi. Aidha, ikumbukwe kuwa hata kazi za fasihi simulizi zinaweza kuhifadhiwa kwa maandishi. Kazi za fasihi zikipatikana kwa wingi, walimu watafanikiwa kupata kazi zinazolingana viwango tofauti vya wanafunzi wao.

**6.0 Hitimisho**

Makala hii imejikita kujadili jinsi fasihi haipaswi kutazamwa kama somo tu bali pia kama nyenzo ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Kwa hivyo, makala imeonesha kuwa fasihi ni nyenzo muhimu ya kukuza uwezo wote unaotarajiwa kukuzwa katika mtaala huo wa kisasa. Hata hivyo, Tumeonesha namna fasihi inavyoweza kufaa kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo kutokana na hoja mbili muhimu: Kwanza, ni kukuza stadi za karne ya 21 ambazo zinamwezesha mwanafunzi kufaa katika maisha ya sasa ambayo yanategemea maendeleo ya kiuchumi zaidi. Pili, ni kutoa fursa ya kudhihirisha utumikaji wa stadi na maarifa wanayojifunza wanafunzi katika mazingira halisi ya nje ya darasa. Kutokana na hali hii, makala imeonesha jinsi utekelezaji fanisi wa mtaala unaoegemea uwezo utatoa suluhisho kwa tatizo lililopo katika nyuga za kiinsia.

Aidha, utekelezaji sahihi wa mtaala unaoegemea katika uwezo, unapaswa kuzingatia ufundishaji wa vipengele vyote vya mtaala huu. Miongoni mwa vipengele hivi ni pamoja na uwezo wa jumla, masuala mtambuka na mitazamo na thamani. Vipengele hivi vinapaswa kufundishwa katika kila somo. Zaidi ya hayo, ni lazima mwalimu asisitize na ajenge mazingira ya utendaji wa vipengele hivyo katika maisha halisi. Aidha, makala hii imejadili pia baadhi ya changamoto za utumizi wa fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo na kutoa mapendekezo ya nini kifanyike kutatua changamoto zilizobainishwa. Hata hivyo, kuna mambo yakutilia maanani kwa walimu na wanafunzi kwa ujumla. Mosi, mwalimu anapaswa kuwa mfano mzuri wa kuigwa katika kila stadi. Pili, kuandaa, kusoma na kutumia kazi za kifasihi tofauti wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Tatu, kuwapa kazi nyingi wanafunzi hasa za kuwasilisha na kuwapa muda wa kujiandaa

kwa ajili ya uwasilishaji wa kazi husika. Nne, kila mwanafunzi apewe na ajue majukumu yake wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Tano, ufundishaji wa mwingiliano wa kitamaduni usipuuzwe. Sita, lugha mama itumiwe tu pale inapohitajika kama vile katika upangaji wa kazi za jozi na makundi na urekebishaji wa kazi ambazo hazishugulikiwi ipasavyo.

**Marejeleo**


Abida, F. I. N. (2016). Critical thinking skills to literary works: A method of teaching language through literature. *JEES (Journal of English Educators Society)*, *1*(1), 1-148.

Al Odhayani, A. na Ratnapalan, S. (2011). Teaching Communication Skills. *Canadian Family Physician*, Juz. *57* (10): 1216-1218.

Assey, P na wenzake. (2007). *Environment at the Heart of Tanzania's Development: Lessons from Tanzania's National Strategy for Growth and Reduction of Poverty (MKUKUTA)*. Natural Resource Issues Series No. 6. International Institute for Environment and Development. London, UK.

Bhaskar, R., Danermark, B., & Price, L. (2017). *Interdisciplinarity and wellbeing: A critical realist general theory of interdisciplinarity*. Routledge.

Boni, A., na Lozano, J. F. (2007). The Generic Competences: An Opportunity for Ethical Learning in the European Convergence in Higher Education. *Higher Education*, Juz. *54* (6): 819-831.

CBSE (2002). *21st Century Skills*. Central Board of Secondary Education, Shiksha Kendra, Delhi

Croce-Galis, M., Hardee, K na Gay, J. (2014). *Kuongeza Ushahidi Unaojulikana kwa Kuzuia Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) Miongoni mwa Wasichana na Wanawake [Scaling up evidenceinformed HIV Prevention for Adolescent Girls and Young Women]," What Works Brief*. Washington, DC: Population Council and What Works Association, Inc.

Croce-Galis, M., Hardee, K., & Gay, J. (2014). Scaling up evidence-informed HIV prevention for adolescent girls and young women. *Policy Brief. Washington DC: Health Policy Project*.

Dornyei, Z. (2007). *Research Methods in Applied Linguistics*. Oxford University Press.

Duhan, R. (2015). The Relationship between Literature and Society. *Language in India*, *15*(4): 1- 192

Education, C. B. S (2020). *21st Century Skills*. The Secretary. Delhi: Preet Vihar: Central Board of Secondary Education.

Fahim, M na Haghani. M (2012). Sociocultural Perspectives on Foreign Language Learning. *Journal of Language Teaching and Research*, Juz. 3(4): 693-699.

González, J. M.F na Wagenaar. R (2003). Quality and European Programme Design in Higher Education. *European Journal of Education*, Juz. 38(3): 241- 251.

Hapsari, A. (2011). Literary Competence for the Teaching of Literature in Second Language Educational Context. *Journal of English and Education (JEE)*, Juz. *5*(1): 29-36.

Huda, H. S na Bushra, S. M. A (2021). Problem-Solving Skill in Language Teaching. *International Journal of Research in Medical Sciences & Technology*, Juz. 11: 60-73.

Jyotsna, J na Dwarakanath. T, (2018) Teaching Life-Skills Through Literature. *International Journal of Research and Scientific Innovation (IJRSI)*, Juz. 5(6): 73-75.

Kabombwe, Y. M., na Mulenga, I. M. (2019). Implementation of the Competency-based Curriculum by Teachers of History in Selected Secondary Schools in Lusaka District, Zambia. *Yesterday and today*, Juz. 22: 19-41.

Kaplan, A. (2016). Lifelong Learning: Conclusions from a Literature Review. *International Online Journal of Primary Education*, Juz. *5*(2): 43-50.

Lan, M.T.Q (2020). Graduate Generic Competences from the Perspective of VNU Employers. *Journal of Teaching and Learning for Graduate Employability*, Juz. 11(1): 131-145.

Lekawael, R. F. J. na Rafli, Z. (2018). The Cultural Values in Texts of English Coursebooks for Junior High School in Ambon, Moluccas-Indonesia. *Advances in Language and Literary Studies*, Juz. *9*(2): 24-30.

Matos, C. L na Afsarmanesh, H (2008). *Concept of Collaboration.* Hershey: IGI Global

Mlaga, K. W. (2021). Ufundishaji na Ujifunzaji katika Nyuga za Kiinsia: Hatari Iliyopo Inakabiliwa? *Jarida la Mnyampala*, Juz. 2(1): 106-119.

Mlaga, W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Nakano, T. C na Wechsler, S. M (2018). Creativity and Innovation: Skills for the 21st Century. *Estudos de Psicologia (Campinas)*, Juz. 35(3): 237-246.

Nosratinia, M na Zaker. A (2014). Metacognitive Attributes and Liberated Progress: The Association Among Second-Language Learners' Critical Thinking, Creativity, and Autonomy. *Sage Open*, Juz. 4(3): 1-10.

Nsengimana, V. (2021). Implementation of Competence-Based Curriculum in Rwanda: Opportunities and challenges. *Rwandan Journal of Education*, Juz. 5(1): 129- 138.

Nzima, I. (2016). Tutors' Interpretations of Competence-Based Curriculum in Tanzania: Implications for practice in teacher education. *Journal of Education of the University of Dar es Salaam.*

REB (2015). *Competence-Based Curriculum*: Summary of Curriculum Framework Pre-primary to Upper Secondary 2015. WordCore Communications Limited.

Shute, V. J., Wang, L., Greiff, S., Zhao, W., & Moore, G. (2016). Measuring problem solving skills via stealth assessment in an engaging video game. *Computers in Human Behavior*, *63*, 106-117.

Tung, C. A., na Chang, S. Y. (2009). Developing Critical Thinking Through Literature Reading. *Feng Chia Journal of Humanities and Social Sciences*, Juz. *19*(1): 287-317.

UNICEF (20219). *Global Framework on Transferable Skills*. United Nations Plaza, New York: UNICEF.

Wambui, T. W., Kibui, A. W., na Gathuthi, E. (2015). Communication Skills, Students Coursebook. *Advances in Language and Literary Studies*, Juz. 1(1): 1-9.